TANGAZO LA SERIKALI NA. 297 la tarehe 19/4/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89)*

SHERIA NDOGO YA AFYA, USAFI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO, YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma ya kuzoa taka.

"ada ya uchafuzi wa mazingira" maana yake ni malipo yanayotakiwa kulipwa kwa Halmashauri na kampuni, viwanda, kikundi, mtu binafsi na taasisi ambazo shughuli zao zinasababisha uchafuzi wa mazingira; kwa kuzingatia kanuni ya mchafuzi hulipa (*Polluter Pay Principle (PPP)*).

"adha" maana yake hali yoyote mbaya yenye kuleta madhara juu ya afya ya watu na viumbe hai kwa ujumla;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake kitu chochote kinacholiwa na binadamu na inajumuisha maji na dawa;

"chanzo cha maji" maana yake ni eneo lolote ambalo limetengwa kwa ajili ya kuwa chanzo cha maji kwa matumizi ya jamii na itajumuisha visima, mito, chemchemi, vijito, na maeneo yote yanayopatikana maji;

"choo bora" maana yake ni choo chochote cha maji chenye sakafu inayosafishika, banda imara la kudumu, limeezekwa, lina mlango imara, bomba la kutolea hewa chafu na lenye mfuniko kwenye tundu la choo na shimo salama na safi kwa ajili ya kutupa kinyesi na mkojo wa binadamu, lililojengwa kwa vifaa vya kudumu;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro;

"uhifadhi wa mazingira" maana yake ni utunzaji endelevu wa ardhi, mimea, hewa, viumbe hai na visivyo hai na vyanzo vya maji unaoozingatia masharti na maelekezo yatakayotolewa na Afisa Mwidhiniwa chini ya Sheria ya Ndogo hii au Sheria nyingine yoyote;

"jengo la biashara" maana yake jengo lolote lililojengwa na kuidhinishwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanyia biashara iliyokusudiwa;

"kaya" maana yake mtu mzima anayejitegemea mwanamke au mwanaume, na mtoto au watoto inayoishi aidha kwenye nyumba nzima au ndani ya chumba kimoja kwenye eneo la Halmashauri;

"kero au chukizo" maana yake ni kitu chochote ambacho kipo katika hali yoyote iwe kinatumika, kimewekwa, kimejengwa, au ni kichafu kiasi cha kusababisha:

(a) hatari kwa viumbe na maisha ya binadamu

(b) harufu mbaya au harufu ya kuudhi au kuleta kinyaa;

(c) kuzaliana kwa wadudu hatari kama vile inzi,

mende, sisimizi, panya, nyoka, nyuki, kunguni au viumbe wengine hatari;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

"kikundi cha mazingira" maana yake ni kikundi chochote cha watu kilichosajiliwa kufanya usafi na usimamizi wa mazingira na udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;

"kikundi cha usafishaji" maana yake kikundi cha watu kilichosajiliwa kufanya shughuli za usafi wa mazingira na hasa za udhibiti wa uharibifu wa mazingira katika maeneo ya Halmashauri;

"kizimba cha taka" maana yake ni eneo maalum lililotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu;

"kituo cha maji machafu" maana yake ni sehemu maalumu iliyotengenezwa kwa ajili ya ukaguzi wa mfereji ambao una mfuniko usioruhusu hewa kutoka;

"kuchakata taka" maana yake ni kuzichambua, kuzitenganisha na kuzibadili kuwa kitu kingine chenye manufaa kwa jamii;

"bwawa la maji taka" maana yake ni bwawa lililojengwa kwa madhumuni ya kuhifadhi na kutakasa maji taka yanayotokana na kuosha vyombo, matumizi ya vyoo na bafu, kufua nguo, kuosha nywele au shughuli zozote maeneo ya bishara, nyumbani na viwandani;

"magonjwa ya mlipuko" maana yake ni magonjwa yanayotokea kwa muda mfupi ya kuambukiza na kuenea kwa haraka na kuathiri watu wengi ndani ya muda mfupi, magonjwa hayo ni kama vile kupooza, kipindupindu, kuhara, surua na homa ya matumbo;

"maji taka" maana yake maji yenye mchanganyiko wa kinyesi, mkojo, na maji kutoka masinki ya kuogea,

kutema mate na kunawia mikono, pamoja na maji yenye mchanganyiko wa vitu vingine vyenye asili ya chemikali au visisvyo na chemikali;

"mazingira" yanajumuisha mazingira ya binadamu ikiwa ni pamoja na hewa, ardhi, maji, hali ya hewa, sauti, mwanga, harufu, ladha, viumbe vidogo, mambo ya kibiolojia ya wanyama na mimea, rasilimali za kitamaduni na sababu za kiuchumi za kijamii na inajumuisha mazingirya asili au kujengwa na jinsi wanavyoingiliana;

"mifugo" maana yake ng'ombe, punda, nguruwe, mbuzi, mbwa, kondoo, kuku na wanyama wengine wote wafugwao na binadamu kwenye eneo la Halmashauri;

"misitu" maana yake ni eneo la ardhi ambalo limefunikwa angalau kwa asilimia 10 na miti, uoto wa asili au uliopandwa, au asilimia 50 au zaidi ya vichaka na miti inayoota au ambayo itajumuisha na yote ya misitu ya hifadhi ambayo itatangaza chini ya sheria za misitu na mazao yote ya misitu ikijumuisha majani na nyasi ndani ya eneo la Halmashauri;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi chini ya Sheria Ndogo hii;

"taka" maana yake ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani kwa wakati huo na uwepo wake katika eneo hilo unaweza kusababisha chukizo la kiafya na kuhatarisha afya ya jamii;

"taka hatarishi" maana yake ni taka zote zenye sumu au kemikali;

"taka ngumu" maana yake ni vitu visivyo majimaji vitokanavyo na shughuli za majumbani, mitaani,

biashara, viwandani na kilimo; pia ni pamoja na takataka za mabaki ya chakula na matunda, za ujenzi na ubomoaji, ufyekaji bustani, shughuli za madini, mizoga na mabaki ya magari mabovu;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ada na ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii;

Mamlaka ya Halmashauri

4.-Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya-

(a) Kusimamia utekelezaji wa shughuli za usafi afya na mazingira.
(b) Kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kufuata kanuni za afya, usafi na kutunza mazingira;
(c) Kuteua Wakala kwaajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira kwa niaba ya Halmashauri kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.
(d) Kufanya ukaguzi ili kubaini endapo kanuni za afya, usafi na utunzaji wa mazingira zinazingatiwa ndani ya eneo la Halmashauri.
(e) Kumchukulia hatua za kisheria mtu yoyote anayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi.
(f) Kuingia mkataba na mtu yeyote, taasisi au Kampuni kutelekeza shughuli za usimamizi wa afya, usafi na mazingira.

Usafi wa mazingira

5.-(1) Kila mtu anawajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) jengo lake, makazi anayoishi au eneo lake la biashara linasafishwa kikamilifu;
(b) taka ngumu zote ikiwa ni pamoja na mifuko ya plastiki zitakusanywa, kuhifadhiwa na kupelekwa katika eneo lililoruhusiwa na Halmashauri;
(c) maji taka yanaelekezwa ndani ya mfumo wa maji taka;

(d) anakuwa na choo bora;
(e) atashiriki siku ya usafi ambayo ni Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi
(f) mfereji wa maji unaomzunguka au kupita kando ya nyumba yake au eneo la biashara yake, kiwanja chake inakuwa safi wakati wote
(g) nyumba yake, eneo lake la biashara au kiwanja chake hakina mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu na mazingira
(h) Anakuwa na chombo imara chenye mfuniko kwa ajili kuhifadhia taka ngumu kabla hazijachukuliwa kwa ajili ya kwenda kutupwa katika eneo lilotengwa kwa ajili ya kuhifadhi taka;
(i) anatunza na kuhifadhi vyombo vya kuhifadhia taka vinavyowekwa na Halmashauri;

Usimamizi wa vyanzo vya maji

6.-(1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa:
(a) kusimamia na kulinda vyanzo vya maji;
(b) kupanda miti isiyonyonya maji katika vyanzo vya maji kwa kuzingatia maelekezo ya kitaalamu;
(c) kuchukuwa hatua za kisheria dhidi ya mtu yeyote atakayeharibu chanzo cha maji, kuchafua chanzo cha maji au kushindwa kushiriki katika shughuli za kuhifadhi vyanzo vya maji bila sababu ya msingi;

(2) Mtu yoyote -
(a) Atakayena nawa, oga, fulia nguo au kunywesha mifugo karibu au kwenye chanzo cha maji kama vile chemchem, kisima au chanzo kingine chochote cha maji;
(b) Atakaye jenga boma la mifugo karibu au kuruhusu mkojo ya mifugo au maji machafu yatokanayo na zizi la mifugo yake kuelekea

karibu na chanzo cha maji;

(c) Atakaye fuga au kuchunga mifugo ya aina yoyote, ndani ya chanzo cha maji

(d) Atakaye anzisha na kufanya shughuli za aina yoyote ndani ya mita 60 kutoka kwenye chanzo cha maji

(e) Atakaye lima, kata miti, chunga mifugo, jenga, fanya jambo lolote katika umbali wa mita 60 kutoka chanzo cha maji;

(f) Atakaye jimilikisha eneo la chanzo cha maji asili

(g) Atakaye elekeza mabomba ya maji machafu kwenye mto, bwawa, kisima, mfereji, chemchem au sehemu yoyote ambayo ni chanzo cha maji

(h) kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama au viumbe vingine vilivyo hai;

(i) Atakaye weka kitu chochote chenye sumu kwenye chanzo cha maji ambayo yanatumiwa na binadamu au kiumbe chochote chenye uhai.

(j) Atakuwa ametenda kosa.

Ada ya uzoaji na utupaji taka

7.-(1) Kutakuwa na ada ya uzoaji na utupaji taka ambayo itatozwa na Halmashauri kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa mazingira kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Ada ya uzoaji taka italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi na italipwa kwa wakala au Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo kwa njia ya kieletroniki na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka

(3) Iwapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo Halmashauri itamchukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani

Wajibu

8.-(1) Kila mtu, mmiliki wa kiwanda na mmiliki wa nyumba anawajibu wa-

(a) kutotiririsha au kumwaga au kuruhusu au kusababisha kutiririka au kumwagika kwa maji taka barabarani, uchochoroni, kwenye mifereji, au sehemu yoyote isiyotengwa kwa ajili ya kuhifadhi maji taka

(b) kujenga mifereji na karo kwa ajili ya kuhifadhi maji taka

(c) Kutoruhusu taka kama vile vumbi, maganda, moshi na nyingine zinazofanana na hizo kuwafikia watu na viumbe wengine na kuleta madhara

(d) kunyonya maji taka pale karo la kuhifadhi maji taka linapojaa

(e) Kutosababisha harufu mbaya itakazosababisha kero kwa wakazi wa eneo lolote la Halmashauri.

(2) mtu yoyote, mmiliki wa kiwanda na mmiliki wa nyumba atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa.

Taka hatarishi

9.-(1) Mtu yeyote, kampuni, wakala au taasisi hairuhusiwi kuchoma taka hatarishi bila kutoa taarifa kwa Halmashauri

(2) Halmashauri au wakala anaweza kuteketeza taka hatarishi kwa gharama ya shilingi elfu hamsini kwa tani moja ya taka.

Utengenezaji na uuzaji vyakula

10. Mfanyabiashara wa chakula ataandaa, kuchoma, kupika, kuchemsha na kuuza chakula cha aina yoyote mahali popote au kwenye nyumba yoyote ikiwa ametimiza masharti na kanuni za afya.

Uuzaji wa vyakula

11.-(1) Mtu yeyote anayeendesha biashara ya vyakula vya kupikwa au kukaangwa atakuwa na wajibu wa kuhakikisha vyakula hivyo vinahifadhiwa kwenye sanduku safi na lenye kuzuia inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Mtu yeyote anayeuza vyakula visivyopikwa

atatakiwa kuuza vyakula hivyo vikiwa juu ya meza.

Usalama wa matumizi ya maji

12.-(1) Kila mkazi anapaswa kuhakikisha kwamba maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama bila kujali yanatoka kwenye chanzo gani cha maji.

(2) Kila mmiliki wa kisima atapaswa kuhakikisha maji ya kisima yamepimwa na yamethibitika ni salama kabla ya kuruhusu yatumiwe na binadamu na wanyama.

Uzuiaji wa shughuli wakati wa magonjwa ya mlipuko

13.-(1) Mkurugenzi anaweza kuzuia yoyote isifanyike kwa kutangaza kwa njia ya kipaza sauti, maandishi au kupitia vyombo vya habari endapo atakuwa na sababu ya kuamini kwamba shughuri hiyo inaweza kusababisha kuenea kwa magonjwa ya mlipuko na kuleta athari kwa maisha ya binadamu

(2) Mtu yoyote atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa.

Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (2) Halmashauri inaweza kuviharibu vyakula vitakavyokamatwa wakati wa katazo

(3) Halmashauri haitahusika na gharama za uharibifu zozote zitakazotokea isipokuwa kama uharibifu huo utakuwa umesababishwa kwa uzembe wa Afisa wa Halmashauri.

Upimaji wa afya

14.-(1) kila mhudumu wa hoteli, migahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba za kulala wageni, grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atatakiwa kupima Afya kila baada ya miezi sita.

(2) Mmiliki wa biashara atakayeruhusu mhudumu yeyote kufanya kazi bila kupimwa afya yake atakuwa ametenda kosa.

Ukaguzi

15.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kuingia katika jengo lolote kuanzia Saa moja na nusu asubuhi hadi Saa kumi na moja kamili jioni kwa lengo la

kufanya ukaguzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Mkurugenzi anaweza kutoa muda wa siku thelathini kwa mmiliki wa jengo au biashara kurekebisha mapugufu yatakayoonekana kipindi cha ukaguzi kwa mujibu wa kanuni hii.

(3) Mkurugenzi anaweza kufunga biashara yoyote au jengo ambalo limekaguliwa na kukutwa limekiuka masharti ya Kanuni hizi.

Udhibiti wa ubebaji kokoto, mawe na mchanga

16. Mtu yeyote atakayesafirisha mawe, mchanga au kokoto katika eneo la Halmashauri atahakikisha kuwa chombo anachotumia kusafirisha kimefunikwa ili kuzuia kumwagika kwa mawe, mchanga au kokoto hizo na kuchafua mazingira.

Wajibu wa kupanda miti

17. Kila mmiliki wa jengo la makazi au biashara, na mmiliki wa shamba atakuwa na wajibu wa kupanda miti kwenye jengo au shamba analomiliki.

Ushirikishaji wa jamii katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira

18. Halmashauri inaweza kuingia mkataba na mtu yeyote, taasisi, kikundi binafsi au asasi ya kiraia, ndani ya Halmashauri katika ngazi ya Mtaa, Kata au Wilaya katika kuboresha bustani, eneo la wazi na uhifadhi wa mazingira.

Tathimini ya athari kwa mazingira na jamii

19.-(1) Miradi yote inayotekelezwa ndani ya Halmashauri haitaaendelezwa bila kufanyiwa tathmini ya athari ya mazingira

(2) Kila mpendekezaji wa mradi atawajibika kulipa Halmashauri asilimia kumi ya thamani ya mradi ikiwa ni gharama ya tathimini ya athari za mazingira juu ya mradi husika.

Udhibiti utupaji wa taka kwenye vyombo vya usfariri

20.-(1) Kila mmiliki wa chombo cha usafiri wa umma ataweka chombo au kifaa maalumu kwaajili ya kuhifadhia taka za abiria.

(2) Watumiaji wa vyombo vya usafiri binafsi au vya

umma hawataruhusiwa kutupa taka nje ya vyombo wanavyotumia na taka zote zitawekwa kwenye chombo cha kuhifadhia taka kilichomo kwenye chombo husika.

(3) Mtu yoyote atakayekiuka masharti ya kanuni hii atakuwa ametenda kosa.

Uanzishwaji wa Vikundi Jamii (*CBOs*)

21. Halmashauri itakuwa na jukumu la kuhamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira baada ya kuingia mkataba na Halmashauri

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

22.-(1) Kila mmiliki wa nyumba ana wajibu wa kuhakikisha kwamba:

(a) nyumba yake ina choo safi, imara kwa matumizi ya wakazi wa nyumba hiyo;
(b) anaweka sehemu maalum ya kunawia mikono ikiwa na maji safi na sabuni.

(2) Choo kinatakiwa kijengwe umbali wa mita sitini kutoka chanzo chochote cha maji.

Masharti ya ujenzi wa vyoo vya umma

23. Vyoo vya umma vitakavyojengwa kwenye eneo lolote la Halmashauri vitatakiwa view vya kudumu na vitatakiwa kuwa na

(a) Matundu yasiyopungua mawili kwa wanawake na mawili kwa wanaume
(b) Mfumo madhubuti wa maji na uwepo wa maji ya kutosha yaliyo safi na salama;
(c) Chombo cha Kuhifadhia maji ya akiba;
(d) Bafu la wanaume na wanawake;
(e) kuwepo na Sehemu ya haja ndogo kwa wanaume; na
(f) kuwepo na chombo maalumu chenye mfuniko cha kuhifadhia taka zisizoweza kusukumwa na maji.

Vyoo vya muda katika mikusanyiko

24.-(1) Ni wajibu wa mtu yeyote, kikundi au taasisi yenye lengo la kukusanya watu kwa madhumuni ya mkutano au sherehe au mkusanyiko wowote kuweka vyoo vya muda endapo eneo hilo hakuna choo cha kudumu

(2) Mtu yeyote, kikundi au taasisi inayotaka kuweka choo cha muda itatatakiwa kuomba idhini kutoka Halmashauri kabla ya kuweka choo hicho.

Vyoo katika majengo ya biashara

25. Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 23 ya Kanuni hizi, kila mmiliki wa jengo la biashara atatakiwa kujenga vyoo vyenye kwa ajili ya matumizi ya wateja wake.

Uteuzi wa Wakala

26.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua Wakala wa kusimamia utekelezaji wa kanuni hii ikiwemo kukusanya ada kwa niaba ya Halmashauri

(2) Wakala atakayeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hii atakuwa na wajibu wa

(a) Kukusanya, kwa niaba ya Halmashauri, ada mbalimbali zinazohusiana na afya, usafi na usimamizi wa mazingira, katika eneo lake alilopangiwa na kwa viwango vilichoidhinishwa chini ya Sheria Ndogo hii.

(b) kukusanya ada kwa kutumia mfumo wa kielekitroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

(c) Kutekeleza masharti yote ya mkataba wake na Halmashauri

Makosa

27. Mtu yeyote atakaye;

(a) Tupa taka au uchafu wowote au kuacha taka au uchafu kwenye nyumba, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au eneo linalopakana na nyumba yoyote au ardhi yoyote au karibu na maeneo ya nyumba au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo;

(b) au kujaribu kumzuia au atamshawishi mtu au kundi la watu kumzuia Afisa Mwidhiniwa asitekeleze wajibu wake chini ya Sheria Ndogo hii
(c) Osha magari, kufua, kunywesha mifugo na kukoroga dawa za mimea ndani ya mito, mabwawa au ndani ya chanzo au kisima kinachotumika kwa matumizi ya binadamu;
(d) Atapika vyakula pembezoni ya barabara au nje ya majengo mengine
(e) Atauza vyakula maeneo yasiyo rasmi kwa biashara hiyo;
(f) Kushindwa kuhifadhi chakula kwenye kabati safi lililofunikwa na lenye kioo;
(g) Atafanya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo, katika maeneo yasiyotengwa kwa shughuli hizo;
(h) Atavuta Sigara hadharani au kwenye vyombo vya usafiri
(i) Atatema mate hovyo au kutema mate barabarani au hadharani;
(j) Ataacha chombo cha usafiri katika hali ya uchafu;
(k) Ataenda haja ndogo au kubwa kwenye maeneo mengine tofauti na chooni;
(l) Atachunga mifugo kwenye eneo lolote lililopandwa miti au misitu iliyohifadhiwa;
(m) Atalima au kukata miti katika vyanzo vya maji, milima, kando ya njia, makorongo na sehemu nyingine zozote zinazohifadhiwa ili kupunguza mmomonyoko wa udongo.
(n) Atachoma taka hovyo ndani ya eneo la Halmashauri.

Adhabu

28. Mtu yeyote atakayevunja masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana

na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

kufifilisha kosa

29. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha Shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa

## JEDWALI LA KWANZA

(*limetengenezwa chini ya kanuni ya 7(1)*)

### SEHEMU A: ADA YA UZOAJI WA TAKA

| Namba | Aina ya Biashara | Ada kwa mwezi (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Viwanda vikubwa | 500,000 |
| 2. | Viwanda vya kati | 200,000 |
| 3. | Viwanda vidogo | 50,000 |
| 4. | Vituo vya mafuta | 50,000 |
| 5. | Taasisi za Umma | 80,000 |
| 6. | Migahawa midogo, | 30,000 |
| 7. | Migahawa mikubwa | 100,000 |
| 8. | Vituo vya chakula kwa abiria wa vyombo vya usafiri | 150,000 |
| 9. | *Mini market,* | 20,000 |
| 10. | *Super market* | 30,000 |
| 11. | Maduka ya dawa za binadamu (wauzaji wa jumla/jumla na rejareja) | 30,000 |
| 12. | Maduka ya dawa muhimu (wauzaji wa rejareja) | 6,000 |
| 13. | Nyumba ya kulala wageni yenye Baa na jiko | 30,000 |
| 14. | Nyumba ya kulala wageni pekee | 10,000 |
| 15. | Baa yenye jiko | 50,000 |
| 16. | Baa pekee | 15,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 297 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 17. | Karakana | 100,000 |
| 18. | Gereji za magari | 20,000 |
| 19. | Seremala | 10,000 |
| 20. | Mashine za kusaga na kukoboa | 10,000 |
| 21. | Duka la jumla | 10,000 |
| 22. | Duka la reja reja | 6,000 |
| 23. | Saluni aina zote | 6,000 |
| 24. | Baba/Mama Lishe | 10,000 |
| 25. | Machinga | 6,000 |
| 26. | Wachoma/wapikaji nyama ya nguruwe | 6,000 |
| 27. | Wakaanga Chipsi ,Kuku, Ndizi, Mishikaji | 10,000 |
| 28. | Magenge ya vyakula (sokoni) | 6,000 |
| 29. | Bucha ya nyama/samaki | 6,000 |
| 30. | Nyumba za kuishi yenye kaya moja/ familia moja | 6,000 |
| 31. | Kila kaya/Mpangaji kwenye nyumba ya kuishi yenye wapangaji | 3,000 |
| 32. | Hospitali | 80,000 |
| 33. | Kituo cha Afya | 40,000 |
| 34. | Zahanati | 15,000 |
| 35. | Maabara za binadamu/Wanyama | 15,000 |
| 36. | Shule za msingi na sekondari | 80,000 |
| 37. | Ofisi za Bima ya magari/Majengo za watu binafsi n.k | 15,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 38. | Taasisi zisizo za kiserikali | 15,000 |
| 39. | Taasisi za mikopo | 20,000 |
| 40. | Kituo cha habari (Radio, TV) | 20,000 |
| 41. | Benki | 80,000 |
| 42. | Hoteli | 80,000 |
| 43. | Duka la dawa asili | 6,000 |
| 44. | Mashine za kukamua Alizeti | 10,000 |
| 45. | Stoo | 10,000 |
| 46. | Ghala | 10,000 |
| 47. | Duka la Vifaa vya ujenzi | 10,000 |
| 48. | Duka la Vifaa vya umeme | 6,000 |
| 49. | ATM (ikiwa haiku kwenye tawi la benki husika) | 20,000 |
| 50. | Duka la simu na vifaa vya simu | 6,000 |
| 51. | Fundi simu, TV, Computer, Radio n.k | 6,000 |
| 52. | Duka la jumla na Rejareja | 10,000 |
| 53. | Wakala wa huduma za kifedha (Tigo,Holotel Mpesa,Airtel n.k) | 6,000 |
| 54. | Duka la vitabu | 6,000 |
| 55. | Wakala wa mabasi (Wakatisha tiketi-ofisi) | 6,000 |
| 56. | Duka la nguo, viatu, mabegi | 6,000 |
| 57. | Wakamua juisi ya Miwa | 6,000 |
| 58. | Glosari | 6,000 |
| 59. | Ukumbi wa starehe | 50,000 |
| 60. | Jumba la kucheza Kamari (Casino) | 50,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 297 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 61. | Wachezeshaji Kamari (slot, mashine, Betting) | 10,000 |
| 62. | Duka la vifaa vya pikipiki | 6,000 |
| 63. | Duka la kuuza pikipiki, Toyo, Bajaji | 15,000 |
| 64. | Duka la vipodozi | 6,000 |
| 65. | Fundi pikipiki | 6,000 |
| 66. | Wauza magari (Show room) | 30,000 |
| 67. | Duka la vifaa vya magari | 10,000 |
| 68. | Chuo kikuu (*University*) | 200,000 |
| 69. | Chuo cha kati (*college)* | 100,000 |
| 70. | *Education center* | 20,000 |
| 71. | Vituo vya kulelea watoto (*Day care*), wanafunzi 1-20 | 6,000 |
| 72. | Vituo vya kulelea watoto (*Day care*) wanafunzi 21 na kuendelea | 15,000 |
| 73. | Duka la vioo (*Aluminium*) | 10,000 |
| 74. | *Car wash* | 10.000 |
| 75. | Duka la samani | 10,000 |
| 76. | Duka la matairi | 10,000 |
| 77. | Duka la kuuza baiskeli | 6,000 |
| 78. | Kumbi za kuoneshea video | 6,000 |
| 79. | Kumbi za mazoezi (*GYM*) | 10,000 |
| 80. | Nyumba za ibada (Msikiti, Kanisa) | 10,000 |
| 81. | Sehemu za kulaza magari | 10,000 |

*Tangazo La Serikali Na. 297 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 82. | *Hostel*, watu 1-20 | 10,000 |
| 83. | *Hostel* , watu 21 na kuendelea | 15,000 |
| 84. | Duka la pembejeo za kilimo,mifugo, vyakula vya mifugo | 10,000 |
| 85. | Stoo ya mkaa | 6,000 |
| 86. | Duka la kuoka mikate | 30,000 |
| 87. | Duka la *ice cream* | 6,000 |
| 88. | Fundi nguo (Cherehani) | 6,000 |
| 89. | Duka la virainishi (*Lubricant*) | 6,000 |
| 90. | Vilabu vya pombe ya kienyeji | 6,000 |
| 91. | Kliniki | 15,000 |
| 92. | Fundi viatu (*shoe shine*) | 3,000 |
| 93. | Dobi | 3,000 |
| 94. | Mashine za kuchomelea (Welding) | 6,000 |
| 95. | Wauza CD | 6,000 |
| 96. | Wauza mbao | 10,000 |
| 97. | Maduka ya mitungi ya gesi | 6,000 |
| 98. | Duka la nafaka jumla | 10,000 |
| 99. | Duka la nafaka rejareja | 6,000 |
| 100. | Biashara ya vyuma chakavu | 6,000 |
| 101. | Sonara | 6,000 |
| 102. | Wafanyabiashara sokoni | 6,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 103. | Uzoaji mwingine ambao haujatajwa | 10,000 |

SEHEMU B: ADA YA KUTUPA TAKA DAMPO

| Namba | Aina ya Biashara | Ada kwa tani moja (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Viwanda vikubwa | 50,000 |

JEDWALI LA PILI

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 29*)

KUFIFILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kwamba mnamo tarehe……………ya mwezi……………..Mwaka ……………………….nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kanuni ya ………………………ya Sheria Ndogo ya Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ya Mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo Tarehe…ya Mwezi……………Mwaka…….

Jina………………………………..…..

Saini………………………………..….

Mbele ya:

Jina……………………………………..

wadhifa……………………………………

Saini……..……………………………..

Tarehe: ………………………………….

Muhuri/Lakari ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio liliopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri mnamo tarehe 28 mwezi 2022. Mbele ya

ALLY HAMU MACHELE
*Mkurugenzi wa Halmashauri*
*Halmashauri ya wilaya ya Morogoro*

PASCAL MWENDISHULE KIHANGA
*Mstahiki meya*
*Halmashauri ya manispaa ya Morogoro*

NAKUBALI

**L.S**

Dodoma
02 februari, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi -Ofisi ya Raisi*
*Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa*